**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**April 2024**
**Dodoma**

**Mkuu wa Shule: 0746420986**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0755826451**
**Shule ya Sekondari: KAREMA**
**S.L.P.155, TANGANYIKA**
**Tarehe .13/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAREMA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA MKOA KATAVI MWAKA WA MASOMO 2024/2025.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari **KAREMA** ipo umbali wa Kilometa 130 Magharibi mwa Mji wa **MPANDA**. Usafiri wa basi kutoka mjini **MPANDA** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **MIZENGO PINDA** Nauli ni Shilingi **9000/=** mpaka shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **…………...**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…………** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sketi mbili za darasani rangi ya kahawia (brown) kitambaa cha suti Esteem original Na. 1. Mashono ya sketi ni linda box linda nane, linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto, urefu wa sketi ni kifundo cha miguu. Sketi fupi hazitakiwi kabisa.
ii. Mashati mawili meupe aina ya tomato mikono mirefu yenye “collar” na mfuko kwa kila shati.
iii. Tai mbili rangi ya kahawia (brown)

iv. Kwa watakaovaa **hijab**, ni **majuba mawili** ya rangi nyeupe **yawe marefu yafunike kifua cha mwanafunzi, pia yawe marefu kufunika kifundo cha mikono akisimama. Pia, Majuba mawili ya rangi ya bluu Bahari kwaajili ya kushindia**.
v. Raba nyeusi, Jezi ya rangi ya Pink (Full kits yaani bukta na T - shirt). Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo.
vi. Truck – Suit rangi ya dark blue yenye mistari ya rangi nyeupe pembeni.
vii. Viatu vyeusi vya kufunga kwa Kamba pea mbili, vyenye visigino vifupi (muundo kama viatu vya kiume)**.**
viii. Soksi nyeupe jozi mbili (02) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi.
ix. Sweta moja rangi ya kijani kibichi lenye nembo ya shule.
x. T – Shirt mbili rangi ya Dark Blue na T-shirt moja rangi ya Kijani Tanesco aina ya Spoti, ziwe na nembo ya shule. T- shirt zisiwe na urembo wowote.
xi. Sketi mbili rangi ya dark blue ya kushindia kitambaa cha suti Esteem original Na. 1. Mashono ya sketi ni linda box linda nane, linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto, urefu wa sketi ni kifundo cha miguu. Sketi fupi hazitakiwi kabisa.

**2.2 <u>Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-</u>**

i. Madaftari 12 counterbook Quire 3
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator; kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na uchumi.
vi. Godoro la sponji (2 ½ x6) .
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya kijani kibichi, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya pinki pembe nne*;*
viii. Nguo za ndani za kutosha mpya (Chupi kuanzia Sita na kuendelea), Underskits/ Shimizi, Sidiria nne (04) na za kulalia (night dress) na Tight kuanzia Nne (04).
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

## C: VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA

Mwanafunzi anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo kulingana na tahasusi husika;

**Muhimu:1. kutokana na umbali wa safari, Vifaa vya usafi vinaweza kupatikana kwenye maduka yaliyo jirani na shule.**

**2.Sanduku kwa usalama safarini na shuleni. Inashauriwa ununue sanduku kubwa la BATI (Tranker) la kutosha vifaa vyako vyote lenye kufuri sehemu mbili.**

**3. Spring file kwaajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi**

**4. Kumbuka kuja na kanga au kitenge jozi moja.Tofauti na hapo, nguo nyingine za nyumbani haziruhusiwi kabisa**

**5. Mwanafunzi anashauriwa aje na BIMA YA AFYA**

- **VIFAA VYA USAFI**

**CBG**

(i) Jembe moja na mpini wake
(ii) Hard broom (fagio ngumu ya plastiki)
(iii) Fyekeo
(iv) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 1 (kwa Mwaka)

**HGE**

(i) Jembe moja na mpini wake
(ii) Soft broom
(iii) Fyekeo
(iv) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 1 (kwa Mwaka)
(v) Reki

**HGK**

(i) Mopa yenye Kamba tambi na kindoo chake
(ii) Fagio ya Chelewa
(iii) Fyekeo
(iv) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 5 (kwa Mwaka)

**HGL**

(i) Jembe na mpini wake
(ii) Squizer
(iii) Fyekeo
(iv) Toilet scrubing brush
(v) Hard broom
(v) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 5 (kwa Mwaka)

**HKL**

(i) Jembe moja na mpini wake
(ii) Soft broom
(iii) Fyekeo (v) Reki
(iv) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 5 (kwa Mwaka)

**HGFa**

(i) Jembe moja na mpini wake
(ii) Soft broom
(iii) Fyekeo
(iv) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 5 (kwa Mwaka)
(v) Hard broom

**HGLi**

(i) Jembe na mpini wake
(ii) Squizer
(iii) Fyekeo
(iv) Toilet scrubing brush
(v) Dawa ya kusafishia vyoo aina ya Careline Disifectant Lita 5 (kwa Mwaka)
(vi) Hard broom

### 2.3 Michango ya Shule

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB**. Michango jumla ya **Tsh.80, 000/=** iingizwe katika akaunti ya shule iliyopo katika Benki ya **NMB (Account No. 61901200071)** inayoitwa **Karema Secondary School Capitation Account** kisha tuletee **Bank payin-slip** ukiwa umeandika jina lako na mchanganuo wa malipo nyuma ya karatasi hiyo.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi wa shule anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

ANIZA EDWARD MALOBA

MKUU WA SHULE
23 APR 2024
SHULE YA SEKONDARI KAREMA TANGANYIKA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0746420986**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0755826451**
- **Mwandamizi Malezi: 0755909415**

**ORODHA YA VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI.**

1. **IDARA YA KISWAHILI**

I. VITABU VYA UCHAMBUZI USHAIRI

**JINA LA KITABU** **MWANDISHI**.

- **Kimbunga** - H. Goro
- **Fungate ya uhuru** - M.S. Khatibu
- **Chungu tamu** - T.A. Mvungi

RIWAYA.

- **Vuta n'kuvute** - S.A. shafi
- **Usiku utakapokwisha** - M. Msokile
- **Mfadhili** - H. Tuwa

TAMTHILIYA

- **Morani** - E. Mbogo
- **Nguzo mama** - P. Muhando
- **Kivuli kinaishi** - S. Mohamedi

II. **Kiswahili Sekondari** - kidato cha V & VI - Oxford.

III. **Kiswahili Sekondari – Kidato cha Tano (TIE)**

IV. **Kiswahili Sekondari – Kidato cha Sita (TIE)**

**2. ENGLISH DEPARTMENT**

**LANGUAGE – I -**

1. Ashel, N. (2009) **Advanced Level English A Practical Approach**. DSM.
2. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form Six) - DSM 3. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form five) – DSM.
4. English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.
5. Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

**LANGUAGE –II-**

1. Ashel, N.(2011), **Advanced Level Literature**. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.
2. **Advanced Level Literature**, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.
3. Achebe, A.(1966) **A man of the People**.
4. Ayi Kwei Armah (1968), **The Beautyful Ones Are Not Yet Born.** 5. Ibsen, H. (1882), **An Enemy of the People,** EA-DSM

**3. GEOGRAPHY DEPARTMENT**

1. (Colin Buckle), **LANDFORMS IN AFRICA**
2. C.R. KOTHARI), **RESEARCH METHODOLOGY**
3. (H.C. TRURAN), **A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS**
4. (Goh cheng Leong.Gillian.C. Morgan), **HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY**

**4. HISTORY DEPARTMENT**

**I. READING LIST FOR HISTORY ONE.**

1. Hallert, R.(1983). **Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers**. Nairobi, Kenya.
2. July, R.W. (1992). **A History of the African People**, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
3. Illife, J. (1995). **Africans, the History of the Continent**. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.

4. Manning, P. (1990). **Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade**, Cambridge University Press.

**II. READING LIST FOR HISTORY TWO**.

1. Nelson throne **Essential modern world history**
2. **History of 21st century** (World history) (Oxford)
3. H.L. Peacock. **A History of Modern Europe 1789-1981** seventh Edition (2010)
4. **The History of Modern World** (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

## 5.GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. **General Studies for Advanced Level Certificate**;
2. Mgaywa, B.M. **General Studies for Advanced level 3rd Ed**.
3. Joannes BigirwaMungu & Sospeter.M. Deogratias. **Understanding Advanced Level general** Studies**; Advanced** Secondary School Education;

## 6. BASIC APPLIED MATHEMATICS

1. Basic Applied Mathematics for Secondary School.
2. Basic Applied Mathematics Review.

3 . Basic Applied Mathematics (TIE)

## 7. ECONOMICS REVISION BOOKS

1. Gupta S.L. and Chaturved D.D (2003) managerial Economics, Text and cases. 2. Macro and Micro Economics by Jigan, Business Account Volume One and Two by Frank wood

## 8. CHEMISTRY AND BIOLOGY DEPARMENT

1.S. Chand's Biology for Class xi and Class xii by Dr. P. S. Verma& Dr. B. P. Pandey

1. Biological science by D. J. Taylor,
2. New understanding Biology for Advanced level fourth edition by 2. Glenn and

Susan Tool. 4. A- Level Chemistry 4th Edition, RAMSDEN EN (2002)

3. Chand, S, Conceptual Chemistry for Class XI.

**KAREMA SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 155,**
**MPANDA,**
**12th June,2023**

Ref. No ………………………………………………
**PART A:**
To the Medica Officer,
……………………………………………………
……………………………………………………
**REF:**…………………………………………………………………………………………
………………..
Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for being a full-time student.
The examination should include the following categories (a-d).
(i) Eyesight (ii)Hearing (iii)Speech (iv)Limbs (v)General Diseases (vi)Leprosy (vii)Epilepsy.
(viii) Neurosis (ix) Other serious diseases e.g., Asthma, T. B., etc.

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)
I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time advanced secondary school education.

(i) Eyesight……………………………………
(ii) Hearing……………………………………
(iii) Speech…………………………………………..
(iv) General diseases……………………………….
(v) Leprosy…………………………………………….
(vi) Epilepsy……………………………………………
(vii) Neurosis…………………………………………..
(viii) Other serious diseases e.g.Asthma…………
(ix) T. B. ……………………………………………………
(x) Pregnancy…………………………………………………

Comments……………………………………………………………………………………………

………………………….....      Name…………………………………………………………..

date…………….......  Signature……………………………

**STATION**……………………………………**DESIGNATION**………………………
………….
**N.B, I request this form to be returned to the school in a sealed envelope**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**

**SHULE YA SEKONDARI KAREMA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA.**

**Passport ya karibuni**

## A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:

1. JINA LA MWANAFUNZI: ………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA: ………………….
3. MAHALI ALIPOZALIWA:
   MKOA…………………………WILAYA…………………..................
   KIJIJI …………………………….. ANAPOISHI KWA SASA: ……………………………
   MKOA........................ WILAYA......................................
   KIJIJI.............................
4. URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA: ..............................
   KABILA …………………………
5. DINI/ DHEHEBU: …………………………
6. SHULE ALIYOTOKA: …………………………………
7. NAMBA YA MTIHANI (CSEE); ……………………….
8. SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE:…………………………… WILAYA………………………. MKOA: ………………………

## B KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.

MIMI ……………………………………………..KIDATO CHA…………MWAKA……………..MCHEPUO WA……………

Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi

kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.

TAREHE………………………. SAINI: …………………………

**C. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:**

**MWANAFUNZI**:

Mimi:……………………….......................................................................................... nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

TAREHE………………………. SAINI: ..............................

**D. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI;(ANDIKA MAJINA MATATU)**

1. JINA LA BABA: ………………………………MAHALI ANAPOISHI: ………………………………

YUKO HAI /AMEFARIKI …………………….........

KAZI YA BABA: …………………...........................

SIMU YA BABA: ………………………………………………..

S.L.P ……………………… MJI…………………….

5. JINA LA MAMA:……………………..........................

MAHALI ANAPOISHI ……………………. YUKO HAI/AMEFARIKI……………………… KAZI YA MAMA:…………………… ……………..

SIMU YA MAMA.....................................

S.L.P. ............................MJI...........................................

**ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI**:

6. JINA LA MLEZI WA KIUME……………………………….................................

MAHALI ANAPOISHI.............................

UHUSIANO............................ SIMU: ..........................

S.L.P. ..........................MJI............................................................

7. JINA LA MLEZI WA KIKE ....................................................

MAHALI ANAPOISHI..........................

UHUSIANO................................ SIMU.........................................

S.L.P. ..........................MJI............................................................

## E. MZAZI/MLEZI (AZAJE SEHEMU HII):

Mimi…………………………………………………….nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi……………………………………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama
Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri.
Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule.
Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.
TAREHE:
……………………………………SAINI:……………….

## F: SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:

Ndugu wa karibu watatu (3) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.
**Majina Matatu Mfano**: JUMA MUSA HASANI

| **JINA** | **UHUSIANO:** | **NAMBA ZA SIMU:** |
|---|---|---|
| 1. ………………............... | …………… | ............................... |
| 2. …………………............. | ……………. | ............................... |
| 3. ………………………… | …………….. | …………………… |
| 4………………………… | …………….. | …………………… |